



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**



Kumb.Na.TTC/02/63/VOL.VI/59

29/08/2023

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma anawatangazia watazania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya kazi ya dereva daraja II. Tangazo hili ni kutokana na kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb.Na.FA.170/571/01"A"/55 cha tarehe 26/06/2023 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

### **DEREVA DARAJA LA I- NAFASI 1**

#### **SIFA ZA MWOMBAJI**

Awe na ufaulu/cheti cha kidato cha nne na leseni ya Daraja G, E au C<sub>1</sub> ya uendeshaji magari ambayo amefanya kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali, Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya Uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali, Waombaji wenye Cheti cha majaribio ya ufundi Daraja II watafikiliwa kwanza.

#### **MAJUKUMU YA KAZI YA DEREVA**

- I. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- II. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- III. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
- IV. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- V. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika Daftari la Safari.
- VI. Kufanya usafi wa gari.
- VII. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

#### **MSHAHARA**

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani ngazi ya Mshahara ya TGS B

#### **MASHARTI YA WAOMBAJI**

- I. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18.
- II. Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa na nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA).
- III. Waombaji waambatishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani, namba za simu za kuaminika pamoja na majina matatu ya wadhamini (referees) wa kuaminika.

- IV. Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya taaluma, nakala ya cheti cha kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa husika.
- V. Picha ndogo moja 'Passport Size' ya hivi karibuni landikwe majina nyuma.
- VI. Testmonial.Provisional results, Statement of result, hati ya matokeo za kidato cha nne na sita, yaani form IV na form VI results slips **havitakubaliwa**.
- VII. Maombi yaweze kuandikwa kwa lugha ya kiswahili fasaha au kiingereza fasaha na yatumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma.
- VIII. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **06/09/2023 saa 9:00 Alasiri**.

**MAOMBI YOTE YATUMWE KWA NJIA YA POSTA KWA ANWANI IFUATAYO;-**

MKURUGENZI MJI,  
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA,  
S.L.P 73,  
**TUNDUMA.**

**LIMETOLEWA NA;-**



*Philemon M. Magesa*

**MKURUGENZI**  
**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**